# Wilaya ya Shule ya Francis Howell

# Kanuni ya Maadili Mema ya Mwanafunzi

Francis Howell
SCHOOL DISTRICT

HOME SCHOOL COMMUNITY

LEARNING TOGETHER

# Utangulizi

## Mazingira Mema, Yenye Heshima ya shule ni muhimu kwa elimu

Kila mtu anatamani shule yake iwe mahali pa kukaribisha, pazuri, na penye heshima. Kwa kufanya kazi pamoja, wanafunzi, wazazi/walezi, wafanyakazi, na jamii wanaweza kufanya shule yao kuwa mahali pazuri pa mafunzo. Mwalimu mkuu anawajibika kudumisha mazingira mazuri ya kusoma. Wanafunzi wanaweza kusaidia kwa kukumbuka:

- Kuwa salama, kuwajibika, na kutulia
- Kuwaheshimu wanarika na watu wote wazima
- Kuheshimu mali zote za shule
- Kuwa shuleni na darasani kwa wakati unaofaa
- Kuwa tayari kwa darasa, pamoja na kazi na vifaa
- Kushiriki katika masomo yao
- Kuwa wakarimu na watumie lugha inayofaa
- Kuvaa vizuri
- Kufuata kanuni za shule na za waalimu wao
- Kuheshimu na kukubali utofauti kati ya watu
- Kuonyesha jinsi wanavyohisi au wanachohitaji kwa njia zinazosaidia na zinazofaa
- Kutatua kutoelewana kwa njia zinazokubalika

## MSAADA WA KITABIA

Shule nyingi za FHSD zimeanza kutumia njia ya Mfumo wa Usaidizi Unaotumia Mbinu Kadha wa Kadha kufunza tabia zinazokubalika na kuwasaidia wanafunzi ambao wanahitajimsaada wa ziada.

## ELIMU YA TABIA

Shule nyingi za FHSD zina mipango iliyowekwa vizuri ya Elimu ya Tabia ambayo inafanya kazi ili kuunda "jamii inayojali ya wanafunzi" kwa sifa nzuri za kitabia katika vijana kupitia maendeleo ya kiakili, kijamii na kimaadili. Wilaya ina shule tatu (3) ambazo zilipokea uteuzi wa Missouri School of Character na shule mbili (2) ambazo ziliweza kutambuliwa kwa National School of Character

## Kiongozi Ndani Yangu

Shule moja ya FHSD imeanza kutumia mpango wa Covey's Leader In Me kama njia ya kukuza uongozi katika wanafunzi. Kulingana na kitabu cha *The 7 Habits of Highly Effective People*, mpango wa Leader in Me (Kiongozi Ndani Yangu) huwaandaa wanafunzi na ujasiri wa kibinafsi na ujuzi wanaohitaji ili kufanikiwa katika uchumi wa karne ya 21. Shule za Leader in Me (Kiongozi Ndani Yangu) huripoti kwa mfululizo utamaduni ulioimarika wa shule na kupungua kwa ujumla kwa matatizo ya kinidhamu.

Kanuni za Maadili Mema ya Wanafunzi wa Shule ya Francis Howell inaelezea tabia ya wanafunzi ambayo huzingatiwa kuwa haifaii au sumbufu. Inatoa pia taratibu mbalimbali

ambazo zinaweza kutumiwa kuzuia tabia kama hiyo na hatua za kinidhamu ambazo zinaweza kuchukuliwa ikiwa wanafunzi watahusika katika tabia zilizotajwa. Wilaya ya Shule ya Francis Howell pia inaunga mkono matumizi ya taratibu za kuingilia kati ambazo zinawapa wanafunzi mwongozo, mwelekezo, na msaada wa kufanikiwa shuleni.

## Miongozo ya Nidhamu Darasani

Kuunda mahusiano mema na wanafunzi ndio msingi wa usimamizi fanifu wa darasa. Waalimu wana wajibu wa kudumisha mazingira ya darasa yanayofaa kwa elimu. Majadiliano ya kuimarisha jamii yanahimizwa na wilaya kama njia ya kuunda jamii inayojali ambayo inajitunza na kujifuatilia. Madarasa yenye mahusiano thabiti na mema kati ya wanafunzi na walimu hukuza mazingira husishi ya elimu. Tunaamini kwamba masomo hufanyika vizuri katika jamii ya elimu ambapo wanafunzi wanashirikiana kati yao na kukuza ujuzi wa kuwafanya kuwa tayari kwa jamii na kufanya kazi. Usumbufu darasani au mchanganyiko wa usumbufu ikiwemo, lakini haijakomea kwa, kuongea sana, kuwa mbali na kiti, kurusha vitu, kuwasumbua wengine, matumizi mabaya ya vifaa vya elektroniki, kupitisha vijikaratasi vya manukuu na/au vitendo vingine ambavyo vinatatiza mchakato wa elimu haukubaliwi.

### Hatua za Hatua ya Kinidhamu

| Tatizo | Hatua |
| --- | --- |
| Tatizo la kwanza | Mwalimu anaongea na mwanafunzi |
| Tatizo linaloendelea | Mwalimu anampa mwanafunzi onyo<br>Mwalimu anaweza kumwelekeza mwanafunzi katika chumba cha urafiki/nafasi ya kujituliza.<br>Mwalimu anaweza kuwasiliana na wazazi/walezi |
| Tatizo halijatatuliwa baada ya onyo | Huenda mwalimu akachagua kumzuia au kuita mkutano wa kutatua tatizo pamoja na mwanafunzi na/au wazazi/walezi |
| Tatizo halijatatuliwa baada ya kumzuia au mkutano. | Mwalimu anamwelekeza mwanafunzi kwa ofisi ya mwalimu mkuu |

### Sera ya Kuchelewa

Uzuiliwaji utatolewa na mwalimu/mwalimu mkuu wakati wanafunzi wanafika darasani baada ya kengele kulia, na kufika kuchelewa kwa dakika 10. Mara za kuchelewa ambazo zinasababisha uzuiliwaji zitabainishwa katika kiwango cha jengo. Baada ya kuchelewa kwa mara kadhaa, wanafunzi wanaweza pia kuelekezwa ofisini kwa hatua zaidi za kinidhamu.

# Makosa ya Kitabia na Viwango vya Kutoa Majibu

Sera za Wilaya ya Shule ya Francis Howell zimebuniwa ili kuchangia mazingira mema ya elimu yanayotumiwa kwa usalama, ufanisi na mafanikio ya kibinafsi. Kwa hivyo, chati kwenye kurasa zinazofuata zitaonyesha makosa ya kitabia kama yanavyofafanuliwa na Wilaya ya Shule ya Francis Howell na kiwango kinacholingana cha nidhamu.

Viwango vya matokeo vinaweza kutofautiana kati ya shule ya msingi na ya sekondari. Ni muhimu kukumbuka kwamba lengo kuu la nidhamu ni kufunza tabia inayohitajika, inayofaa na kuzuia tabia isiyofaa baadaye.

Makosa ya Kitabia yaliyoorodheshwa katika kurasa zinazofuata yatapitiwa na wanafunzi wote kwa njia ambayo inafaa umri. Wazazi wanahimizwa kupitia makosa hayo na watoto wao.

Safari za shule au shughuli zingine za shule, zikiwemo zile za nje ya majengo ya shule, ziko chini ya utawala wa mfanyakazi aliyeteuliwa wa shule. Sera na masharti yote ya Wilaya yanatumika wakati wa shughuli hizi iwe ni wanafunzi wa shule ya msingi au wa sekondari wanaohusika (shule ya kati na ya upili). Wanafunzi watawajibika kulingana na Kanuni za Maadili Mema ya Wanafunzi kwa makosa yanayofanyika wakati wa safari na shughuli za nje ambazo zinafanyika nje ya majengo ya FHSD.

FHSD inaweza na itachukua hatua za kinidhamu kwa matukio ambayo yanafanyika nje ya kampasi ikiwa kuna uhusiano (yanaunganika) na shule au ikiwa tukio hilo linasababisha usumbufu kwa mazingira ya shule.

KANUNI ZA MAADILI MEMA HAZIWEZI KUTARAJIWA KUORODHESHA AU KUELEZEA KILA MOJA YA KOSA AMBALO LINAWEZA KUHITAJI MATUMIZI YA HATUA ZA KINIDHAMU. HATA HIVYO, WILAYA INA HAKI YA KUTEKELEZA MATOKEO YOYOTE AMBAYO YANAWEZA KUFAA CHINI YA HALI HII, KULINGANA NA HALI, UKALI NA MARUDIO YA TABIA HUSIKA.

# Makosa ya Kitabia na Viwango vya Kutoa Majibu

## Kiwango cha 1 - Uingiliaji Kati wa Darasa ukiwa na Nidhamu au bila

- Uingiliaji Kati wa Darasa Ukiwa na Nidhamu au Bila
- Mkutano wa walimu na mwanafunzi na kufundisha tena tabia inayofaa na/au kanuni za darasani
- Mwanafunzi kutumwa katika chumba cha urafiki
- Mawasiliano ya kunena/kuandika na wazazi/walezi yanayohusiana na tabia
- Kukataa upendeleo maalum kama vile motisha au shughuli zilizo zaidi ya mtaala
- Mkutano wa mwalimu/mzazi/mlezi
- Kunyimana mapumziko - nusu/yote (inapaswa kutumiwa tu wakati ambapo hakuna chaguo zingine za kukabiliana na ukiukaji wa kitabia)
- Kufungwa
- Mkutano wa Urejeshaji

**Kiwango cha 2 - Uingiliaji Kati wa wafanyakazi ukiwa na Nidhamu Simamizi au bila**

- Majibu ya Kiwango cha Kwanza na/au Urejeshaji
- Kosa la Kwanza - Kufungwa hadi siku 3 za Kusimamishwa Shuleni
- Kosa la Pili - Hadi siku 5 za Kusimamishwa Shuleni
- Kosa la tatu na Linalofuatilia - Hadi siku 5 za Kuwa Nje ya Shule
- Mkutano wa Urejeshaji

**<u>Kiwango cha 3 - Uingiliaji Kati wa Kina na Nidhamu Simamizi</u>**

- Majibu ya Kiwango cha 1 hadi cha 2 na/au
- Siku kadhaa za Kusimamishwa Shuleni na/au Hadi siku 10 za Kuwa Nje ya Shule (Huenda ukatumia mchanganyiko wa kuwa shuleni na nje ya shule bila kuzidisha siku 10)
- Mkutano wa Urejeshaji

**<u>Kiwango cha 4 - Mikakati ya Kina, Uingiliaji Kati na Usimamizi</u>**

- Kuondoshwa kwa Muda Nje ya Shule Hadi Siku 10 na rufaa wezekano kwa Usikilizaji wa Kamati ya Mienendo pamoja na uwezekano wa siku za ziada za Kuondoshwa Kwa Muda Shuleni hadi siku 180
- Mkutano wa Urejeshaji

**<u>Kiwango cha 5- Uingiliaji Kati wa Kina Pamoja na Uwezekano wa Kuondolewa Shuleni kwa Muda Mrefu na Mikakati ya Kurejeshwa Tena</u>**

- Kuondolewa Shuleni kwa Siku 10 za Lazima na rufaa kwa Usikilizaji wa Kamati ya Mienendo pamoja na uwezekano wa siku za ziada za Kuondoshwa Kwa Muda Shuleni hadi siku 180
- Uwezekano wa Pendekezo la Kufukuzwa Kabisa
- Ukiukaji wa Silaha- Kuondoshwa kwa muda kusikopungua mwaka mmoja (siku 365 za kalenda) au kufukuzwa kabisa, uamuzi ukifanywa kulingana na Mo. Rev. § 160.261

**<u>Tafadhali Kumbuka</u>**

- (Msingi) hutoa viwango vya kutoa majibu ambavyo ni vya shule za msingi pekee.
- Nia, wigo wa athari, na ukali wa tabia utazingatiwa wakati wa kuamua kiwango cha ukiukaji.

## MATUSI/LUGHA ISIYOFAA/LUGHA CHAFU (AL)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuapa, kulaani au kufanya ishara chafu, au kudharau kwa maandishi au maneno ambayo hayakuelekezwa kwa mtu mwingine au kikundi cha watu | • Kiwango cha 1 | • Kiwango cha 2 | • Kiwango cha 3 | | |
| Kuapa, kulaani au kufanya ishara chafu, au kudharau kwa maandishi au maneno ambayo yameelekezwa kwa mtu mwingine au kikundi cha watu | • Kiwango cha 1 | • Kiwango cha 2 | • Kiwango cha 3 | | |
| Lugha isiyofaa ambayo kwa njia nyingine ni jeuri, chafu, yenye dharau, inayozingatiwa kuwa haifai katika mazingira ya elimu au ambayo inasumbua sana kazi ya darasani, shughuli za shule au kazi za shule. | • Kiwango cha 1 | • Kiwango cha 2 | • Kiwango cha 3 | • Kiwango cha 4 | |

## TABIA ZA KIKATILI

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kupiga, kupiga makofi, kusukuma, kujikwaa, kusukumana, kurusha mateke, kutemeana mate au kitendo kingine chochote kisichofaa cha uchokozi kinachofanywa na mwanafunzi mmoja kinachoelekezwa kwa mwanafunzi mwingine ambacho hakihusishi uonevu au unyanyasaji na hakitoi kiwango cha kupigana au kushambuliwa kimwili | • Kiwango cha 1 | • Kiwango cha 2 | • Kiwango cha 3 | • Kiwango cha 4 | |

## POMBE (A)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kumiliki vinywaji vyovyote vyenye pombe; kutumia na/au kuwa chini ya ushawishi wake, au muda mfupi baada ya kunywa vinywaji vyovyote vyenye pombe | | | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |
| Usambazaji wa vinywaji vyenye pombe | | | | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |

## UCHOMAJI MALI (AR)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuwashwa moto, au kujaribu kuanzisha moto | | | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |

## KUSHAMBULIWA KWA KUJERUHI (AS)

Kiwango cha 4 na 5 kinahitaji rufaa kwa watekelezaji wa sheria.

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Cha mwanafunzi au mfanyakazi, anayejaribu kuua au kusababisha majeraha makali ya kimwili—mwanafunzi kutumia nguvu za kimwili na lengo la kusababisha majeraha mabaya ya kimwili. Rufaa kwa watekeleza sheria itafanywa na usimamizi wa shule. | | | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |

## KUSHAMBULIWA BILA KUJERUHI (ANI)

Kiwango cha 4 na 5 kinahitaji rufaa kwa watekelezaji wa sheria.

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Shambulio la kimwili dhidi ya mwanafunzi au mfanyakazi | | | ● Kiwango cha 3 (Msingi) | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |
| Matumizi ya nguvu ya kimwili, ikiwa ni pamoja na matumizi ya kitu, moja kwa moja dhidi ya au kwa kuathiri mwanafunzi au mfanyakazi au mtu mzima yeyote ambaye anatekeleza mamlaka kihalali shuleni au wakati wa shughuli yoyote ya shule | | | | ● Kiwango cha 4 (Msingi) | ● Kiwango cha 5 |

## UONEVU/UONEVU WA MTANDAONI (UONEVU)

Msimbo Mdogo Unaohitajika: BD – Uonevu kwa misingi ya ulemavu, BR – Uonevu kwa misingi ya mbari/asili ya kitaifa, BS – Uonevu kwa misingi ya kijinsia, BSO – Uonevu kwa misingi ya mwelekeo wa kijinsia, BBR – Uonevu kwa misingi ya kidini, BOTH – Uonevu Mwingine

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuogopesha, tabia ya uhasama isiyohitajika au unyanyasaji (ikijumuisha unyanyasaji wa jinai chini ya Sheria ya Shule Salama), ambayo ni ya kurudia au ina uwezekano mkubwa wa kurudiwa na kusababisha mwanafunzi aliye na busara kuogopea usalama wake wa mwili au mali; uwezekano mkubwa wa kurudiwa na kusababisha mwanafunzi mwenye busara kuogopea usalama wake wa mwili au mali; kuingilia kwa kiasi kikubwa utendaji wa kielimu, fursa au faida za mwanafunzi yeyote bila kuacha yeyote; au kukatiza sana utendaji mzuri wa shule. Udhalimu unaweza kujumuisha vitendo vya kimwili, vikiwemo ishara, au udhalimu wa maneno, kielektroniki, au mawasiliano ya kuandikwa, na tishio lolote la kulipiza kisasi kwa kutoa ripoti ya vitendo kama hivyo. “Udhalimu wa mtandaoni” inamaanisha upitishaji wa mawasiliano ikiwemo, lakini haijakomea kwa, ujumbe, matini, sauti au picha kwa njia za vifaa vya kielektroniki vikiwemo, lakini havijakomea kwa, simu, simu pasiwaya au kifaa kingine chochote cha mawasiliano pasiwaya, kompyuta, au ukurasa. Wanafunzi hawataadhibiwa kwa usemi katika hali ambazo usemi umelindwa na sheria | | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |

## MATUMIZI MABAYA YA KOMPYUTA/TEKNOLOJIA (CTM)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kujaribu, bila kujali mafanikio, kupata ufikiaji usioidhinishwa wa teknolojia; kupata maudhui yasiyofaa; kupata kiwango cha juu cha upendeleo bila idhini; udukuzi; kukwepa/kuzima kichujio | | | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |
| Matumizi mabaya ya Akiliunde (AI) ambayo yanasababisha ukatizaji wa mazingira ya kielimu, au shughuli ya shule | | | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |
| Kurekodi vita | ● Kiwango cha 1 (Msingi) | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | | |

## USEMI UNAODHALILISHA

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Ikiwemo, lakini haijakomea kwa, matumizi ya lugha ya chuki (iliyoandikwa au kunenwa) ili kuwadhalilisha watu wengine kwa sababu za umbari, rangi, jinsia, asili ya kitaifa, umri, jamii, ulemavu, dini, mapendeleo ya kingono au mwelekeo wa kingono unaoshukiwa (inaweza pia kusababisha rufaa ya Title IX au Title VI). Hii ni pamoja na tabia, usemi wa kunena, kuandika au wa ishara. Inaweza kuzingatiwa makosa ya Kiwango cha 4 ikiwa itachukuliwa kuwa ni mbaya sana na mwalimu mkuu/mwakilishi. | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | |

## KUTOHESHIMU (DIS)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Maneno, namna ya sauti, ishara za uso, ishara au maonyesho yaliyoandikwa. Huenda ikajumuisha tabia isiyotakikana na wengine na kukataa kuiacha. Labda mwanafunzi kwa mwalimu au mwanafunzi kwa mwanafunzi. | • Kiwango cha 1 | • Kiwango cha 2 | | | |

## TABIA YA KUTATIZA (DB)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Tabia ambayo inakatiza mafundisho na kusoma kwa wanafunzi wengine darasani | • Kiwango cha 1 | • Kiwango cha 2 | • Kiwango cha 3 | • Kiwango cha 4 | |
| Kupiga teke, kurusha, au kuachilia kitu kwa makusudi (ikiwa ni pamoja na snowball) ambayo ina uwezo wa kusababisha usumbufu, kuumia, au uharibifu wa mali na/au kitu hufanya kuwasiliana kimwili na mwanafunzi mwingine au wenzao, wakati kitendo cha kutupa au kuachilia kitu sio sehemu ya shughuli inayosimamiwa au sio kwa ajili ya madhumuni yaliyokusudiwa. | • Kiwango cha 1 | • Kiwango cha 2 | • Kiwango cha 3 | • Kiwango cha 4 | |

## UKIUKAJI WA SHERIA ZA MAVAZI (DCV)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Hali ya mavazi au mwonekano unaokiuka sheria ya mavazi yasiyofaa kwa shughuli za shule na/au zinazotatiza mchakato wa elimu, ikiwemo, lakini haijakomea kwa, kulegeza suruali/ nguo zinazofichua mwili, zinazofichua nguo za ndani, kuvaa viatu vya njumu na/au minyororo, au chapa zisizofaa kwenye mavazi/barakoa (k.m.Zinazodokeza ngono, dawa za kulevya, vinywaji vinavyolewesha, silaha, shughuli haramu, nk.). Huenda waalimu wakuu wakauliza wanafunzi wawaambie wazazi walete mavazi yanayofaa ya kubadilisha. Ikiwa baada ya mwanafunzi kuambiwa abadilishe na kuvaa mavazi ambayo yanatimiza sheria ya mavazi kisha mwanafunzi huyo apatikane tena kuwa anakiuka tena sheria hiyo ya mavazi, hatua za ziada za kinidhamu zinaweza kuchukuliwa. | • Kiwango cha 1 | • Kiwango cha 2 | | | |

## DAWA ZA KULEVYA (D)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Harufu ya bangi, bila ushahidi wa matumizi au kuwa chini ya ushawishi wake, kwa njia inayotosha kusababisha usumbufu kwa mazingira ya masomo | | • Kiwango cha 2 | | | |
| Matumizi ya dawa zozote za kulevya au kuwa chini ya ushawishi wake, ikiwa ni pamoja na bangi | | | • Kiwango cha 3 | • Kiwango cha 4 | • Kiwango cha 5 |
| Umiliki wa dawa zozote za kulevya au vifaa kama hivyo, ikiwa ni pamoja na bangi | | | • Kiwango cha 3 | • Kiwango cha 4 | • Kiwango cha 5 |

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kununua bangi na/au dawa zozote isipokuwa bangi | | | | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |
| Usambazaji au kushiriki dawa za kulevya, ikiwa ni pamoja na bangi kwa au na mwanafunzi mwingine | | | | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |
| Umiliki au matumizi ya, ikiwemo, lakini haijakomea kwa, dawa zisizoagizwa na daktari ni makosa ya Kiwango cha 2. | | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | | |
| Umiliki au matumizi ya dawa ikiwemo, lakini haijakomea kwa, dawa zisizoagizwa na daktari haziruhusiwi. Usambazaji, uuzaji au ununuzi wa (ikiwemo, lakini haijakomea kwa, dawa zisizoagizwa na daktari) au kuwa chini ya ushawishi wa dawa "zinazouzwa kwenye kaunta" zinazosababisha tabia sumbufu kwa mazingira ya elimu, ikiwa ni pamoja na virutubisho. Ikiwa mwanafunzi anahitaji dawa za kununua kwa kaunta kutibu ugonjwa, basi wanafaa kuripoti hali hiyo kwa muuguzi. | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | |

## KUWEKWA HATARINI (EX)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Isiyo na asili ya kingono Kama vile kukojoa mbele umma. | ● Kiwango cha 1 (Msingi) | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | | |

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Hujumuisha kuonyesha makalio na/au sehemu nyeti katika maeneo ya umma au kumvua mtu mwingine au kujivua mwenyewe na kufichua sehemu yoyote ya siri ya mwili na/au nguo za ndani. Kuvuta chini suruali ya mtu mwingine "Pantsing" iko chini ya makosa haya. Inaweza kusababisha kuripotiwa kwa afisa wa masuala ya utiifu shuleni. | | • Kiwango cha 2 | • Kiwango cha 3 | | |

## KUPIGANA (FG)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Mapigano ya pande zote mbili ambayo yamechangia mzozo ama kwa maneno au kwa hatua ya mwili (yaani, kugonga, kupiga ngumi; kunaweza kuhusisha kugonga kwa kutumia kitu, kupiga teke, kuvuta nywele, kukwaruza nk.). | | • Kiwango cha 2 (Msingi) | • Kiwango cha 3 | • Kiwango cha 4 | |
| Mapigano ya pande zote ambayo yanajumuisha majeraha makali ya mwili kwa mtu mwingine. | | | • Kiwango cha 3 (Msingi) | • Kiwango cha 4 | • Kiwango cha 5 |
| Maneneo au hatua za kuwachochea wapigane, ikiwa ni pamoja na kudhihaki, kuwashawishi, kuwachochea, na/au kuwatia moyo wapigane, kuvuruga, au kukiuka sheria zingine za shule, au kurekodi mapigano. | • Kiwango cha 1 (Msingi) | • Kiwango cha 2 | • Kiwango cha 3 | • Kiwango cha 4 | |

## KAMARI (GM)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Shughuli zisizo za mafundisho zinazojumuisha kamari kwenye matokeo yasiyo na uhakika, bila kujali dau; kujihusisha katika mchezo wowote wa kubahatisha ambapo kitu cha thamani halisi au ishara kinaweza kushindaniwa au kupotea. Mifano ni pamoja na, lakini haikomei kwa kamari kwenye matokeo ya shughuli, kazi, mashindano na michezo. | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | | | |

## UNYANYASAJI/UDHALILISHAJI (HI)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Mgusano wa kimwili au wa maneno, lugha ya maandishi au ishara kwa misingi ya jinsia, utambulisho wa kijinsia, kujieleza kijinsia, mbari, rangi, dini, jinsia, mwelekeo wa kijinsia, asili ya kitaifa, ukoo, ulemavu au sifa nyinginezo zinazolindwa na sheria. Mifano ya unyanyasaji haramu ni pamoja na, lakini sio tu, utani wa rangi au maoni; maombi ya upendeleo wa ngono na matunzo mengine ya ngono yasiyokubalika; grafiti; kuitana majina; au vitendo vya kutisha, vitisho au uadui kwa kuzingatia sifa inayolindwa | | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuogopesha ni tabia ya kimakusudi ambayo ingemfanya mtu mwenye hisia za kawaida kuogopa kuumia au kuumizwa. Sio lazima kuthibitisha kwamba tabia hiyo ilikuwa ya ujeuri kiasi cha kusababisha hofu iliyosemwa au kwamba mwathirika alikuwa na hofu kweli. Kitendo chochote ambacho kinakidhi ufafanuzi wa unyanyasaji/kutisha lakini hakielekezwi kwa moja ya makundi yanayolindwa na sheria kinapaswa kuwa chini ya msimbo mdogo wa HOTH-Unyanyasaji Mwingine | | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |
| Inatumiwa kufuatilia madai ya unyanyasaji. Inahitajika kwa ajili ya kutoa ripoti kwa OCR wakati kuna madai ya matukio ya unyanyasaji / vitisho ambapo mkosaji haiwezi kutambuliwa. Msimbo huu unapaswa kutumika wakati wowote mtu anapodai unyanyasaji, lakini hauwezi kuthibitishwa au kupatikana kuwa SIO unyanyasaji. | | ● Kiwango cha 2 | | | |

## KUCHOKOZA (CHOKOZA)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Shughuli ambayo mtu mwenye busara anaamini itaathiri vibaya afya ya akili au ya mwili au usalama wa mwanafunzi au kumweka mwanafunzi katika hali ya kudhalilisha au ya mawazo mengi kwa madhumuni ya kutangulizwa shuleni, uandikishaji, ushirika katika kikundi chochote, darasa, shirika, kilabu au timu ya riadha. Uchokozi unaweza kutokea hata wakati wanafunzi wote wanaohusika ni washiriki wasiolazimishwa. | | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |

## KIFAA KISICHOFAA/KIPENGEE KINACHOCHOMEKA (IO)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuwepo kwa kitu kisichofaa katika mazingira ya shule ikiwa ni pamoja na kiberiti, njiti, kemikali au vifaa vingine vinavyotumika kuwasha au kuanzisha moto. Sio lazima vipengele visivyofaa viwe vinavyochomeka (k.m. bunduki za midoli, visu vidogo vyenye makali chini ya inchi 4, makasha ya makombora , au vipengee vinavyotumika isivyofaa kama vile mawe). | | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | | |

## UTANGAMANO WA KIMWILI USIOFAA

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| MCHEZO WA KIVITA: Kusukumana/kupigana kumbo/kugonga lakini huenda pasiwe na lengo la kuumiza au kujeruhi mtu. Hatua, zinazojirudia, zinaweza kuzingatiwa kama kategoria tofauti. | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | | | |
| Kushika wengine mwili isivyofaa hiyo haifai. | | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | | |

## KUASI UONGOZI ULIOPO (IS)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutoshirikiana na sheria za shule au maagizo ya wafanyakazi wa shule au wanaojitolea | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | | | |
| Kukataa kufumukana wakati wa vita au usumbufu inapoelekezwa na mtu mzima | | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | | |

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kupita bila ruhusa | | ● Kiwango cha 2 | | | |
| Kutofuata itifaki za usalama wa shule, ikiwa ni pamoja na kufungua milango ya nje iliyolindwa ili kuruhusu mtu mwingine kuingia | | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | | |

## UADILIFU (INT)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kusema uwongo - Kutosema kila kitu, kujaribu kudanganya, au kutosema ukweli kwa mtu mzima au mwenzako. | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | | | |
| Ulaghai/Wizi - Kutumia, kuwasilisha, kupata au kujaribu kupata data, maswali, au majibu kwa njia zingine kuliko zile zilizoidhinishwa na mwalimu, pamoja na matumizi yasiyoidhinishwa ya AI. Ina adhabu ya kupata sufuri kwenye mtihani/kazi na mwalimu humwarifu mzazi/mlezi na msimamizi kuhusu tatizo hilo; hujumuisha udanganyifu wa kielektroniki. Matukio kadhaa yanaweza kusababisha kosa la Kiwango cha 2. | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | | | |
| Kughushi - Kuwasilisha kazi za wengine au hati zilizo na sahihi za uwongo | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | | |

## MATOKEO YALIYOKOSEKANA (MCS)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kukosa matokeo yaliyopeanwa na shule | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | | | |

## TABIA YA UZEMBE

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kusababisha uharibifu kwa mali ya mtu mwingine au majeraha au kuhatarisha usalama wa mtu mwingine (ikiwemo, lakini haijakomea kwa matumizi ya vifaa vya kuchezea vya "mshtuko", ukiukaji wa usalama wa maabara, na tabia nyingine za kutojali). Mizaha ya wanafunzi inaweza pia kujumuishwa katika kategoria hii. | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |

## NYINGINE (OTH)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Tabia mbaya ambayo huathiri mpangilio mwema wa shule unaoibuka na kuwa makosa. Huenda kategoria hii ikatumiwa kwa makosa ambayo hayako chini ya moja ya fafanuzi za makosa. | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |

## MATUMIZI MABAYA YA VIFAA VYA KIELEKTRONIKI VYA KIBINAFSI

Uwepo na/au matumizi mabaya ya kifaa cha kibinafsi cha kielektroniki kama inavyofafanuliwa na matarajio ndani ya Kitabu cha Mwongozo cha Maadili Mema ya Mwanafunzi.

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Shule ya Msingi - Kutumia, kuonyesha au kugeukia vifaa vya kibinafsi vya kielektroniki wakati wa siku ya shule. | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | | | |
| Shule ya Katikati - Kutumia, kuonyesha au kugeukia vifaa vya kibinafsi vya kielektroniki wakati wa siku ya shule. | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | | | |
| Shule ya Upili - Kutumia, kuonyesha au kugeukia vifaa vya kibinafsi vya kielektroniki wakati wa siku ya shule, isipokuwa matumizi yawe sehemu ya madhumuni ya kiakademia yanayoidhinishwa na wafanyakazi. | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | | | |
| Kuunda picha za kidijitali, video na rekodi za sauti ambazo zinavuruga mazingira ya kielimu, zinaweka uwezekano wa kuvuruga mazingira ya kielimu, au kukiuka faragha ya wengine. | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | | | |

## UHABIRIBIFU WA MALI/UVUNJAJI (PD)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Uharibifu wa kimakusudi au jaribio la kusababisha uharibifu wa mali (ikiwa ni pamoja na teknolojia) mali ya shule, wafanyakazi au wanafunzi; kurudishwa shuleni kunaweza kuhitajika ili kurejesha mali iliyoharibiwa. | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | | |
| Uharibifu wa mali ya uhalifu, kama inavyofafanuliwa na sheria. Lazima ashirikiane na watekelezaji wa sheria. Kurudishwa shuleni kunaweza kuhitajika ili kurejesha mali iliyoharibiwa. | | | | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |

## TISHIO LA SHULE

Utathmini wa tishio utafanywa ili kujua uhalali na ukali wa tishio hilo.

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Maonyo Yasiyo ya Kweli – Kuanzisha mifumo ya moto ya shule na/au ya onyo zingine, kutoa ripoti ya moto wakati hakuna moto, au kupigia simu 911 kwa onyo lisilo la kweli. | ● Kiwango cha 1 (Msingi) | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | | |
| Kujaribu au kutumia fataki, bomu la moshi, dawa ya pilipili/gesi, MACE, gesi ya kutoa machozi au bomu inayonuka. | | | | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |
| Kuwasiliana na shule au kikundi kikubwa cha vitisho au ripoti ya uwongo (kwa maneno, kielektroniki, maandishi, au kupitia mitandao ya kijamii) kwa madhumuni ya kutisha au kusumbua watu, kuvuruga mazingira ya elimu, au kusababisha uhamishaji au kufungwa kwa mali ya wilaya. Hii inajumuisha tishio la kuleta silaha shuleni | | | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |
| Kufanya tishio la bomu au kutishia kufyatua kifaa cha kulipuka bila kumiliki haswa kwa bomu au kifaa cha kulipuka. | | | | | ● Kiwango cha 5 |
| Umiliki wa bomu au kifaa kingine kinacholipuka | | | | | ● Kiwango cha 5 |

## UZINIFU WA KIJINSIA/UNYANYASAJI WA KIJINSIA (SM)

Ikiwa picha/video ni za mtoto, ni lazima arifa ya utekelezaji wa sheria na huduma za ulinzi wa watoto zifanywe.

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Lugha ya maneno, maandishi, ishara, mfiduo (wa kingono), au kugusana kimwili kwa njia isiyotakikana na ya asili ya kingono. k.m., kubana, kushikana matiti, matako, sehemu za siri, nk. Hii inajumuisha "kutuma ujumbe wa kingono" wa njia ya kielektroniki. | | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |
| Kumiliki picha au rekodi za kingono kwenye eneo la shule au katika hafla zinazofadhiliwa na shule. | | | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |
| Usambazaji wa picha au rekodi za ngono kwenye mali ya shule au katika hafla zinazofadhiliwa na shule; ikiwa ni pamoja na usambazaji wa picha za ponografia. | | | | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |
| Matendo ya kingono kwenye kampasi ikijumuisha kuonyesha mapenzi. | | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |

## KUCHELEWA (TAR)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufika kuchelewa kwa hadi dakika 10. Zaidi ya dakika 10 inachukuliwa kama kukosa shule. | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | | | |

## WIZI (TH)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuchukua kitu, kujaribu kuchukua kitu, au kumiliki kitu ambacho sio chako. | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | | |
| Wizi kwa njia ya uhalifu, kama inavyofafanuliwa na sheria. Lazima ashirikiane na watekelezaji wa sheria. Huko Missouri, wizi wa jinai hutokea wakati thamani ya kitu ni $750 au zaidi. Sehemu ya 570.030 ya RSMo | | | | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |

## TISHIO/UGOMVI WA MANENO

Utathmini wa tishio utafanywa ili kujua uhalali na ukali wa tishio hilo – Ni ya muda tu au ya maana.

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Vitisho vya maneno, vya maandishi na visivyo vya maneno kwa mtu mwingine ambapo hakuna hofu ya kudhuru mwili. | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | | | |
| Makabiliano ya maneno na wanafunzi wengine au watu wazima ambayo yanaweza kujumuisha au kutojumuisha matumizi ya lugha chafu bila kutumia vitisho lakini kusababisha usumbufu wa mazingira ya masomo. | | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | | |
| Vitendo Tete - Vurugu au vitendo vya kutisha vya hali mbaya ambavyo vinatatiza kwa kiasi kikubwa shule, shughuli inayofadhiliwa na shule au shughuli inayosimamiwa na shule inayofanyika nje ya eneo la shule. | | | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Vitisho vya muda mfupi, kama inavyobainishwa na tathmini ya vitisho, ya vurugu kwa mtu binafsi au vikundi vidogo kupitia mtandao wa kielektroniki, wa maneno, maandishi au kijamii. | ● Kiwango cha 1 | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | | |
| Tishio kubwa la kweli, kama ilivyobainishwa na tathmini ya tishio, kuelekea mtu mwingine. Ushirikiane na watekelezaji wa sheria. | | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | |
| Vitisho vikali, kama inavyobainishwa na tathmini ya vitisho, kwa kutumia mitandao ya kijamii (ikiwa ni pamoja na, lakini sio tu kwa Snapchat, Twitter, Facebook, nk.) kuelekea mtu mwingine au kusababisha usumbufu. Inaweza kujumuisha vitisho vya kigaidi. Ushirikiane na watekelezaji wa sheria. | | | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | ● Kiwango cha 5 |

## MIFUMO YA UTOAJI WA TUMBAKU/NIKOTINI (TB)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kumiliki na/au matumizi ya bidhaa yoyote ya tumbaku au kipulizia cha nikotini (yaani, sigara ya kielektroniki). | | ● Kiwango cha 2 | | | |
| Kumiliki na/au kutumia kalamu ya "vape". | | ● Kiwango cha 2 | | | |
| Usambazaji wa vifaa vya nikotini, ikiwa ni pamoja na uuzaji/usambazaji wa vape ya nikotini. | | ● Kiwango cha 2 | ● Kiwango cha 3 | ● Kiwango cha 4 | |

## UTORO (TR)

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutokuwepo darasani au shuleni bila idhini kwa mwanafunzi yeyote bila kujali umri, ikijumuisha sehemu yoyote ya siku zaidi ya dakika 10, inachukuliwa kuwa utoro. Ingawa kwa kawaida kukosa kwenda shuleni humaanisha kutokuwepo ambako wazazi hawatambui, kutokuwepo fulani ambako mzazi anafahamu kutashughulikiwa kwa njia ileile ya kukosa kwenda shuleni; inajumuisha kukwepa au kuondoka kwenye eneo au jengo bila ruhusa. | • Kiwango cha 1 | • Kiwango cha 2 | • Kiwango cha 3 | • Kiwango cha 4 | • Kiwango cha 5 |

## SILAHA (W)

Watekelezaji wa sheria ni lazima wawasilianwe nao unapotumia msimbo huu.

| Tabia | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kumiliki silaha yoyote kama inavyofafanuliwa katika Sera ya Bodi ya FHSD. | | | | | • Kiwango cha 5 |
| Matumizi ya silaha yoyote kama inavyofafanuliwa katika Sera ya Bodi ya FHSD. | | | | | • Kiwango cha 5 |
| Uuzaji, uombaji na/au usambazaji wa silaha yoyote kama inavyofafanuliwa katika Sera ya Bodi ya FHSD. | | | | | • Kiwango cha 5 |

# VIFAA VYA KIBINAFSI VYA KIELEKTRONIKI

## Matarajio ya Shule za Upili

**Matarajio ya Vifaa vya Elektroniki**

Wilaya ya Francis Howell inatambua thamani ya mchakato wa kufundisha na kujifunza. Kwa faida na umakini wa kufundisha na kujifunza shuleni, ni marufuku kwa wanafunzi kutumia vifaa vyao vya kielektroniki, kama vile simu za rununu, wakati wa siku ya shule. Ni marafuku kabisa kwa wanafunzi kuonyesha au kutumia vifaa vyovyote vya kielektroniki wakati wa siku ya shule. Wanafunzi wanaruhusiwa tu kutumia vifaa vya kielektroniki wakati inahitajika na wafanyakazi kwa madhumuni ya kielimu.

## Matarajio ya Shule za Msingi na za Katikati

**Matarajio ya Vifaa vya Elektroniki**

Wilaya ya Francis Howell inatambua thamani ya mchakato wa kufundisha na kujifunza. Kwa faida na umakini wa kufundisha na kujifunza shuleni, ni marufuku kwa wanafunzi kutumia vifaa vyao vya kielektroniki, kama vile simu za rununu, wakati wa siku ya shule. Ni marufuku kabisa kwa wanafunzi kuonyesha au kutumia vifaa vyovyote vya kielektroniki wakati wa siku ya shule na inatawaliwa na masharti yafuatayo.

## Ufafanuzi ufuatao unatumika kwa vifaa vya elektroniki:

Neno '**elektroniki**' au '**vifaa vya kielektroniki**' linamaanisha sehemu yoyote na komponenti zote za elektroniki, vifaa, au zana, ikiwa ni pamoja na lakini sio tu kwa simu za rununu, saa mahiri, mifumo ya mchezo wa video, hedifoni za aina yoyote (ikijumuisha vifaa vya masikio), spika, na kamera.

**KUMBUKA: Haijumuishi** kompyuta, vipakatalishi, au chromebook zinazotumiwa kwa kazi ya darasa. Haijumuishi teknolojia saidizi ambayo imejumuishwa ndani ya hati hii katika sehemu ya mwisho: **Umaalum wa Teknolojia Saidizi.**

## Kanuni za Jumla Zinazotumika kwa Wanafunzi Wote

Kanuni zifuatazo zinazohusiana na kuonyesha au matumizi ya vifaa vya kielektroniki zinatumika kwa wanafunzi wote:

- **Wajibu kuhusiana na Vifaa vya Kielektroniki:** Wanafunzi ambao huleta vifaa vya kielektroniki shuleni hufanya hivyo kwa hatari yao wenyewe na wana wajibu wa kulinda vifaa hivyo dhidi ya uharibifu, wizi, au kupotea. Shule na wilaya haziwajibikii vifaa vya kielektroniki vya wanafunzi.
- **Uundaji wa picha za Kidijitali, Video, na Rekodi za Sauti:** Ni marufuku kwa wanafunzi kuunda picha za kidijitali, video na rekodi za sauti ambazo zinavuruga mazingira ya kielimu, zina uwezekano wa kuvuruga mazingira ya kielimu, au kukiuka faragha ya wengine.
- **Matokeo ya Matumizi Mabaya ya Vifaa vya Elektroniki:** Ikiwa mwanafunzi ataleta

kifaa cha elektroniki shuleni na kiwe kinaonekana, kinasikika, au kinamilikiwa au kinatumiwa na mwanafunzi wakati usioidhinishwa, mwanafunzi huyo anakabiliwa na matokeo yaliyowekwa katika Kanuni ya Maadili (COC) ambapo msimamizi anaweza kuchukua kifaa hicho cha mwanafunzi. Katika tukio ambapo kifaa cha elektroniki kinachukuliwa, msimamizi wa jengo ataripoti mzazi wa mwanafunzi na kurudisha kifaa cha elektroniki kilichochukuliwa kwa mwanafunzi mwishoni mwa siku ya shule ambayo alinyang'anywa

- **Umaalum wa Teknolojia Saidizi:** Vizuizi juu ya vifaa vya elektroniki katika sehemu hii havitumiki kwa vifaa saidizi vya teknolojia ambavyo vinahitajika na mwanafunzi mwenye ulemavu kama sehemu ya Mpango wake Uliobinafishwa wa Elimu ("IEP"), huduma zinazohusiana, au misaada na huduma za ziada. Hali maalum pia inatumika kwa malazi yanayohitajika chini ya mpango wa Sehemu ya 504. Vifaa vya teknolojia saidizi vinavyohitajika na wanafunzi kama ilivyowekwa na mipango yao ya IEP au Sehemu ya 504 vinaweza kutumiwa wakati wa siku ya shule, pamoja na wakati wa darasa, kama inahitajika kuwezesha mafundisho na ushiriki wao, kulingana na mpango wao wa IEP au Sehemu ya 504.
- **Hali maalum pia zinajumuisha:**
  - Wanafunzi wa Kiingereza kwa Wazungumzaji wa Lugha Zingine (ESOL) ambao hutumia kifaa hicho kwa madhumuni ya mawasiliano na mafundisho.
  - Wanafunzi ambao wana Mpango wa Afya wa Mtu Binafsi (IHP) kwa kutumia vifaa vya elektroniki kwa sababu za kimatibabu (kwa mfano: vifaa vinavyohusiana na ugonjwa wa kisukari na moyo).

# PROGRAMU YA A+ YA WANAFUNZI WA SHULE YA UPILI

## Sera ya Raia wa A+ ya Wanafunzi wa Shule ya Upili

Kamati ya Ushauri wa A+ ya Wilaya ya Shule ya Francis Howell inaamini kwamba uraia mwema ni muhimu kwa wanafunzi wanaohitimu na sifa ya A+. Wanafunzi wanaoshiriki katika mpango wa A+ wanaoondoshwa kwa muda wanahatarika kustahiki kwao. **Ustahiki wa A+ unaweza kuathiriwa na matokeo ya nidhamu.** Miaka yote minne ni sehemu ya rekodi ya uraia. Matokeo yafuatayo yatasababisha kuondolewa kwa Programu ya A+:

- Matukio 5 au zaidi ya kuondoshwa kwa muda darasani/shuleni wakati wa taaluma ya mwanafunzi ya shule ya upili (gredi ya 9 hadi 12).
- Kuondoshwa kokote ambako kunasababisha kuondoshwa kwa muda shuleni kwa zaidi ya siku 10 au zaidi.

## Mchakato wa Rufaa ya A+

Mwanafunzi na/au mzazi/mlezi ana haki ya kuomba rufaa ya A+ baada ya kupokea ilani ya makosa ya kuhudhuria au ya uraia. Katika visa vya wasiwasi au kutostahiki:

- Lazima mwanafunzi na mzazi/mlezi aarifu Mratibu wa A+ kwa kumwandikia kuhusu lengo lake la kujadili wasiwasi huo au kustahiki.
- Mratibu wa A+ ataita mkutano wa Kamati ya Rufaa ya A+ ili kuzingatia ustahiki.

- Kamati ya Rufaa ya A+ itasikia ombi na kurudisha uamuzi wake kwa mwanafunzi na mzazi/mlezi. Mtu yeyote anayeomba rufaa anapaswa kukamilisha fomu ya “Rufaa ya A+” ambayo inapatikana kutoka kwa mratibu wa A+ katika shule ya upili ya mwanafunzi. Baada ya kamati ya ukaguzi kupata uamuzi, Mratibu wa A+ ataarifu mzazi/mlezi.

## USTAHIKI WA SHUGHULI ZINAZOATHIRIWA NA MWENENDO

### Viwango vya Kustahiki vya Wilaya ya Shule ya Francis Howell

Mshiriki yeyote wa mwanafunzi anayewakilisha mojawapo ya Shule za Upili za Francis Howell kwa kushiriki katika timu za riadha au vikundi vya maonyesho, pamoja na shughuli za muziki (bendi ya maandamano, mlinzi wa rangi, makundi, kwaya, ngoma msimu wa baridi), shughuli za densi (densi/pommers na mlinzi wa msimu wa baridi), hotuba na mjadala, mchezo wa kuigiza, au mashindano ya kitaaluma (kikombe cha wasomi) lazima afikie viwango vya ustahiki vilivyoainishwa katika Katiba ya MSHSAA na viwango vya ziada vya Wilaya ya Shule ya Francis Howell.

- Wanafunzi wanapaswa kujiepusha na matumizi ya tumbaku yoyote, sigara za kielektroniki (bidhaa za kuvuta), pombe, au dawa haramu/bidhaa zinazodhibitiwa (isipokuwa dawa iliyoagizwa na daktari).
- Wanafunzi ambao wanahudumu katika Programu ya Kusimamishwa Shuleni (ISS) hawaruhusiwi kufanya mazoezi au kushiriki hadi kusimamishwa kwao kutekelezwe. Wanafunzi ambao wanahudumu katika Kusimamishwa kwa Shule ya Nje (OSS) hawataruhusiwa kufanya mazoezi au kushindana hadi kusimamishwa kwao kuhudumiwe na wamejianzisha tena kama mwanafunzi katika msimamo mzuri kwa kuhudhuria siku kamili ya shule siku iliyofuata.
- Mwanafunzi yeyote anayedanganya katika hati zinazohitajika atakuwa wa kufukuzwa kutoka kwa shughuli ambazo wanahusika.
- Ni lazima mwanafunzi awe raia wa shule mwenye kuaminika. Wananchi wa shule wenye kuaminika ni wale wanafunzi ambao mwenendo wao, ndani na nje ya shule, hautaonekana mbaya kwao wenyewe, timu au shule.
- Mwongozo wa Shughuli za Wilaya ya Shule ya Francis Howell (FHSD) hutoa habari nyingi juu ya ustahiki kuhusiana na mwenendo ndani na nje ya shule na miongozo ndani yake itafuatwa na washiriki wote katika shughuli za FHSD.
- Miongozo ya Chama cha Shughuli za Shule ya Upili ya Jimbo la Missouri (MSHSAA) lazima ifuatwe na kuzingatiwa ili kushiriki katika shughuli za FHSD.

## Matumizi ya Pombe na Dawa za Kulevya

Bodi ya Elimu inatambua mgao wake wa majukumu ya afya, maslahi na usalama wa wanafunzi wanaohudhuria Wilaya ya Shule ya Francis Howell. Kwa hivyo, matumizi, mauzo, uhamishaji, umiliki au kuwa chini ya ushawishi wa pombe au dawa za kulevya umepigwa marufuku kwenye majengo ya shule, katika shughuli au matukio yanayofadhiliwa na shule, kwenye safari za

kimasomo, au ndani ya gari lolote linalotumika kuwasafirisha wanafunzi kwa ajili ya wilaya ya shule.

Pombe, kama inavyotumiwa katika Kanuni hii ya Maadili Mema ya Wanafunzi, inaelezewa kama vinywaji vya pombe, vinywaji vya kimea “visivyokuwa na pombe” au dawa zozote zilizowasilishwa kuwa pombe au vinywaji vya kimea “visivyokuwa na pombe”.

Dawa za kulevya, kama inavyofafanuliwa katika Kanuni hii ya Maadili Mema ya Wanafunzi, zinafafanuliwa kama vileo, dawa haramu, dawa zinazoagizwa na daktari, kemikali halali zisizoagizwa na daktari au dawa za kununua kwenye kaunti ambazo zinasababisha kudhoofika, na/au kemikali zinazobadilisha mwili au akili au dawa zinazothibitiwa; au dawa zinazowasilishwa kama vileo, dawa haramu, dawa za kuagizwa na daktari, kemikali halali zisizoagizwa na daktari au dawa za kununua kwenye kaunta ambazo zinasababisha kudhoofika, na/au kemikali zinazobadilisha mwili au akili au dawa zinazouzwa kwenye kaunta zinazotumiwa kwa lengo tofauti na lengo lake; au vifaa vya dawa.

Ijapokuwa sio lengo la Bodi au kitivo cha shule na usimamizi kuzuia elimu ya mtu yeyote anayestahiki katika wilaya ya shule, inatambuliwa kwamba nidhamu nzuri shuleni na uraia mwema shuleni ni muhimu kwa mazingira mazuri ya elimu kufanyika. Sio haki kwa wanafunzi wale wanaotaka kunufaika na nafasi zao za elimu na shughuli kuathiriwa na usumbufu usiofaa unaosababishwa na wanafunzi wengine ambao wametumia dawa za kulevya au pombe au wanaomiliki vifaa hivi.

Mwanafunzi yeyote anayepatikana kuwa chini ya ushawishi au anamiliki pombe au dawa za kulevya anaweza kuondoshwa kwa muda shuleni kwa kipindi cha hadi siku 180 za shule au kufukuzwa shuleni kabisa. Mwalimu mkuu/mwakilishi atawaondosha kwa muda wanafunzi kama hao kwa kipindi cha kwanza cha siku kumi (10) za shule. Kwa makosa ya kwanza ya kumiliki pombe au kumiliki dawa za kulevya, badala ya kuondoshwa kwa muda shuleni kwa siku 10, mwanafunzi huyo anaweza kuchagua kuhudhuria Mpango Mbadala wa Uingiliaji Kati (AIP) ambao uko ndani ya Shule ya Upili ya Francis Howell Union High School.

Katika AIP (Mpango Mbadala wa Uingiliaji Kati), mwanafunzi atahitajika kushiriki katika tathmini ya awali ya uandikishaji iliyokamilishwa na wafanyakazi wa FHU, ambao wataamua ni kozi gani ya matumizi ya dawa/pombe na ushauri nasaha wa kuzuia matumizi mabaya ambao mwanafunzi atakamilisha. Mwanafunzi atahudhuria siku nzima ya shule na atakamilisha kazi zote kutoka kwa kozi zake na kushiriki katika huduma za ushauri na za kuzuia matumizi mabaya ya dawa/pombe. Hii inaweza kujumuisha huduma zinazotolewa na PreventEd au tathmini ya kina ya madawa ya kulevya na uchunguzi wakati wa kuandikishwa kupitia Kituo Kinachopendelewa cha Afya ya Familia pamoja na ushauri wa ufuatiliaji. Wanafunzi wataendelea kupokea msaada kuhusu kutoa maamuzi mema na kuunda uvumilivu baada ya kurudi katika shule yao ya nyumbani. Ikiwa mwanafunzi au mzazi/mlezi hatakamilisha hati zinazohitajika, tathmini au mikutano inayoendelea ya msaada kwa njia ya kuridhisha, kuondoshwa huko kwa kwanza kwa siku 10 kutatekelezwa, na Kamati ya Kusikiliza Mienendo itakutana ili kubainisha adhabu inayofaa na/au siku zaidi za kuondoshwa kwa muda shuleni. Mapendekezo ya adhabu yatapelekwa kwa msimamizi/aliyeteuliwa kwa uamuzi wao na matokeo hayatakuwa chini ya siku 20 za kusimamishwa.

Baada ya kufanyika tena kwa kosa la pili chini ya Kanuni za Maadili Mema ya Wanafunzi, mwanafunzi huyo atashiriki katika Usikilizaji wa Kamati ya Mienendo na ataondoshwa kwa muda shuleni kwa hadi siku 180 za shule au kufukuzwa kabisa.

Kulingana na ukali wa makosa, mwanafunzi aliyepatikana kuwa ameshiriki katika uuzaji, kushiriki au usambazaji wa pombe au dawa za kulevya ataondoshwa kwa muda shuleni kwa hadi siku 180 au kufukuzwa kabisa. Huenda mwalimu mkuu/mwakilishi akawaondosha kwa muda wanafunzi kama hao kwa kipindi cha kwanza cha siku kumi (10) za shule. Usikilizaji wa Kamati ya Mienendo unaweza kufanyika ndani ya kipindi cha kuondoshwa kwa muda cha siku kumi (10) za kwanza ili kubainisha adhabu inayofaa. Pendekezo la adhabu linaweza kuwasilishwa kwa msimamizi/mwakilishi kwa uamuzi wao. Afisa wa kusikiliza kesi za Kamati inayohusiana na Mienendo, kwa uamuzi wao, inaweza kupendekeza mahali mbadala pa elimu - Kituo Mbadala cha Masomo (ALC). Ikiwa mpango huo utakubalika: (1) Ndani ya siku mbili (2) za kuanza kwa ALC, lazima tathmini ya dawa za kulevya ikamilishwe katika Kituo Kinachopendelewa cha Afya ya Jamii. Mwanafunzi huyo atahitajika kushiriki katika vikao vya mashauri ya dawa za kulevya vinavyotolewa na Preferred Family Health.

## Shule Zisizo na Silaha za Vita

Wilaya ya Shule ya Francis Howell inatafuta kutoa mazingira salama ya elimu yasiokuwa na vurugu kwa wanafunzi wake na eneo la kazi kwa wafanyakazi wake. Wilaya inathibitisha kwamba silaha hazina nafasi yoyote kwenye maeneo ya shule.

Wilaya inagundua kwamba ni lazima itii sheria za serikali na jimbo kuhusiana na kuwashughulikia wanafunzi wanaoleta silaha shuleni. Vivyo hivyo, maelezo haya yanatii matoleo ya Sheria ya Kuboresha Shule za Marekani ya 1994, Sheria ya Elimu ya Watu walio na Ulemavu na sheria nyingine husika za serikali na jimbo.

Wilaya inatambua hatari ya madhara ambayo mtu anayeleta silaha za vita shuleni anaweza kusababisha kwake na kwa wengine katika majengo ya shule. Wilaya inagundua umiliki wa silaha kuwa tishio linalotarajiwa la afya, usalama na ulinzi wa wanafunzi, wafanyakazi na watu wengine. Wilaya haitavumilia hatari ya madhara yanayoletwa na mtu anayeleta silaha za vita kwenye majengo ya shule zetu.

### Kwa hivyo Wilaya inasema ifuatavyo:

**UFAFANUZI**

Neno "silaha za vita“ limefafanuliwa kulingana na sheria ya serikali kama ilivyowekwa katika toleo jipya la Sheria ya Marekani ya 18 Sehemu ya 921. Neno "silaha ya vita“ linajumuisha, lakini halijakomea kwa, vitu kama vile:

- Kitu chochote ambacho kimewekwa risasi au silaha isiyokuwa na risasi, fremu ya silaha au mtutu wa silaha na ambao umeundwa, au unaweza kubadilishwa kwa urahisi ili kutoa risasi kwa kitendo cha vilipukaji; au
- Kitu chochote ambacho kinaweza kugeuzwa haraka kutoa risasi kwa kitendo cha

vilipukaji au rafadha nyingine, na ambayo ina mtutu ulio na risasi za angalau kipenyo cha nusu inchi; au

- Kilipukaji chochote, makombora yenye kulipuka au gesi yenye sumu, kama vile: bomu, grunedi, roketi yenye rafadha ya zaidi ya aunsi nne (4); na vifaa vingine kama hivyo kama vinavyotambuliwa chini ya sheria ya serikali; au
- Mchanganyiko wowote wa sehemu zilizoteuliwa au zilizokusudiwa kutumiwa katika kugeuza kifaa chochote kama inavyofafanuliwa katika aya ya B au C ya Sehemu ya Ufafanuzi.

**WANAFUNZI WANAOLETA BUNDUKI SHULENI**

Wilaya haitakubali mwanafunzi kuleta silaha ya vita shuleni. Kwa hivyo, Wilaya itachukua hatua ifuatayo baada ya kubainisha kwamba mwanafunzi ameleta silaha ya vita shuleni:

- Wilaya itamwelekeza mwanafunzi kwa mahakama yanayofaa au mfumo wa mahakama ya watoto; na
- Wilaya itamwondosha mwanafunzi huyo kwa muda shuleni kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja (1) (siku 365) kuanzia tarehe ya makosa hayo, na huenda, kwa uamuzi wake, ikamfukuza mwanafunzi huyo kabisa shuleni. Toleo hili la kuondoshwa kwa muda linaweza kurekebishwa kulingana na hali baada ya nyingine baada ya pendekezo la Msimamizi wa Shule ikiwa Msimamizi atabainisha kwamba hali hizo zinafaa mabadiliko hayo.
- Huenda Wilaya, kwa uamuzi wake, ikampa mwanafunzi aliyeondoshwa kwa muda Chini ya Sera ya Wilaya ya 2620 huduma za elimu katika mazingira mbadala.

**HALI YA KUTUMIKA KATIKA WANAFUNZI WALIO NA ULEMAVU**

Ikiwa mwanafunzi anayebainishwa kuwa anakiuka miongozo hii ya Shule Bila Silaha ni mwanafunzi aliye na ulemavu chini ya Sheria ya Elimu ya Watu Walio na Ulemavu, Wilaya itafuata mahitaji ya serikali na jimbo yaliyowekwa katika sheria na masharti husika. Sheria na masharti kama hayo yaliweka taratibu maalum za kufuatwa wakati mwanafunzi aliye na ulemavu analeta silaha ya vita shuleni. Miongozo hii itatumika kwa wanafunzi walio na ulemavu kwa kadri ambayo matumizi yake inaruhusiwa chini ya Sheria ya Elimu ya Watu Walio na Ulemavu.

**HALI YA KUTUMIKA KATIKA SERA ZA WILAYA NYINGINE**

Sera zingine zote za Wilaya kuhusu silaha, sera za nidhamu au sera za silaha zinazofanana zitaendelea kutumika kama zilivyo kwa sasa au zilivyorekebishwa hapa.

## Miongozo ya Matumizi Inayokubalika ya Mtandao na Intaneti

Ufikiaji wa Intaneti unapatikana katika Wilaya ya Shule ya Francis Howell (FHSD) kwa wanafunzi, walimu, wafanyakazi, wazazi/walezi na wasimamizi. Lazima wanafunzi watumie mawasiliano ya FHSD kulingana na Sera ya Wilaya ya 6320. Wanafunzi wanaruhusiwa kufikia

maelezo yanayohusiana na mtaala na kutafuta mada na dhana ambazo zinakuza uvumbuzi katika elimu.

Kujifunza jinsi ya kuwasiliana kwa njia pepe na kupitia maelezo mengi yaliyo kwenye mitandao ya umma na ya kibinafsi ni ujuzi wa kusoma na kuandika ambao unaunga mkono mafanikio ya mwanafunzi katika karne ya 21. Katika hali nyingine, wanafunzi, wakiidhinishwa na mwalimu wa darasa, wataruhusiwa kuleta teknolojia zao wenyewe kwa madhumuni ya elimu (k.m. vipakatalishi, iPods, iPads, visomaji vya kielektroniki, nk.).

Usalama Wilaya huhakikisha utiifu wa CIPA (Sheria ya Ulinzi wa Intaneti ya Watoto) kupitia matumizi ya ngome na uchujaji. Hata hivyo, wanafunzi wanapaswa kuripoti kwa mwalimu wao au wafanyakazi wengine ikiwa watafikia maelezo ambayo yanawafanya wasijihisi vizuri.

Hatua zifuatazo ZINARUHUSIWA kwenye mitandao ya wilaya:

- Matumizi ya mawasiliano kwa malengo ya elimu pekee
- Kuwasiliana na wengine kwa njia ya heshima na ukarimu
- Kutii sheria za hakimiliki na haki za rasilimali ya akili za wengine
- Kudumisha usiri wa majina ya kibinafsi, nambari za simu, anwani na nenosiri, na kuheshimu usiri huo wa watu wengine

Miongozo hii imetolewa ili ufahamu kuhusu majukumu yako. Msimamizi wa mtandao au mwakilishi aliyeteuliwa wa FHSD anaweza kubadilisha haki za mtandao/kompyuta ikiwa miongozo hii haitazingatiwa.

Hatua zifuatazo HAZITARUHUSIWA kwenye mitandao ya wilaya:

- Kushiriki maelezo ya siri
- Kupeana nenosiri kwa wengine
- Kupeana maelezo ya kibinafsi kwenye Intaneti
- Kunyanyasa, kutukana, au kuwadhuru wengine kwa njia yoyote ile
- Kufikia nyenzo za ponografia/za kinyume cha sheria
- Kujaribu kuruka au kubatilisha mfumo wa usalama
- Kunakili programu kinyume cha sheria
- kuingia kwenye folda, faili au hati za wengine bila
- ruhusa Kujaribu kuharibu data/faili za wengine
- Kutumia mtandao kwa malengo ya kibiashara
- Kutumia lugha chafu
- Kutumia michezo ya Intaneti isiyo ya mtaala
- Kukiuka sheria za hakimiliki au wizi wa maandishi
- Kutumia tovuti zisizoidhinishwa
- Kuharibu mtandao au teknolojia ya Wilaya
- Kupakia virusi, kubadilisha data au wizi wa maelezo yaliyozuiwa

Ukiukaji wa Sera ya Wilaya ya 6320 kuhusu matumizi ya mtandao na intaneti utasababisha hatua za kinidhamu kuchukuliwa ambazo zinajumuisha, lakini hazijakomea kwa, moja au zaidi ya zifuatazo: 1) kusitishwa au kubatilishwa kwa haki za mtandao; 2) kuondoshwa au kubatilishwa kwa ufikiaji wa Intaneti; 3) kuondoshwa au kubatilishwa kwa ufikiaji wa kompyuta;

4) kuondoshwa kwa muda shuleni; au 5) kufukuzwa kabisa.

TAFADHALI KUMBUKA: Ikiwa ungetaka kukataza matumizi huru ya intaneti kwa mwanafunzi wako, tafadhali wasiliana na shule anayehudhuria ili upate fomu inayofaa.

## Adhabu ya Viboko ni Marufuku

Sera ya Wilaya 2670 inasema: Hakuna mtu aliyeajiriwa au kujitolea wa Wilaya atamwadhibu au kusababisha kuadhibiwa kwa viboko mwanafunzi anayehudhuria shule za Wilaya. Mfanyakazi wa Wilaya anaweza kutumia udhibiti unaoeleweka dhidi ya mwanafunzi bila ilani ya mapema ya mwalimu mkuu/mwakilishi ikiwa ni muhimu kujilinda mwenyewe, kudumisha mpangilio, au kuwakinga watu wengine au mali ya Wilaya.

## Miongozo ya Basi

Madereva wa mabasi ya Francis Howell wamevikwa majukumu ya kudumisha mazingira salama na mema katika mabasi ya wilaya.

Ifuatayo ni orodha ya matarajio ya wanafunzi wakiwa ndani ya mabasi ya wilaya:

- Fuata matarajio yote katika Kanuni za Maadili Mema ya Wanafunzi
- Fuata maagizo yote ya dereva wa basi
- Endelea kuketi ukiwa umeangalia mbele ya basi
- Panda na ushuke basi katika vituo vilivyoteuliwa
- Weka sehemu zote za mwili na vitu vyote ndani ya basi
- Watendee wengine kwa heshima (kwa maneno na kimwili)
- Shughulikia basi kwa heshima (hakuna uharibifu wa vitu, kutupa taka, kurusha vitu, kula au kunywa)
- Panda basi ulilotеuliwa

KUMBUKA: Huenda mabasi yote yakafuatiliwa na kamera wakati wowote ule.

Ili kudumisha mpangilio na kutoa mazingira salama, dereva wa basi anaweza kuchukua yoyote kati ya hatua zifuatazo:

- Kuanzisha mkutano na mwanafunzi
- Kuanzisha mkutano na mwalimu mkuu/mwakilishi
- Kuwaelekeza wanafunzi kutii sheria
- Kupangia viti vya basi
- Kupeana maonyo ya tikiti za basi
- Kupeana tikiti za basi

Wilaya itachukulia basi kuwa mwendelezo wa darasa; kwa hivyo, mwenendo wowote mbaya kwenye basi utakuwa na matokeo. Matokeo yanaweza kujumuisha kuondoshwa kwenye basi. Katika hali ambapo ukiukaji ni mkali na/au unatishia usalama wa jumla wa wanafunzi, suala hilo litaelekezwa mara moja kwa mwalimu mkuu/mwakilishi. Mwalimu mkuu/mwakilishi kwa

uamuzi wake anaweza kutekeleza/kuanzisha mpango mbadala wa nidhamu ikihitajika. Mkurugenzi wa Wilaya wa Usafiri na Meneja wa Operesheni za Usafiri watakutana na mwalimu mkuu/mwakilishi kama ilivyoombwa au wakati inahitajika.

# Kamusi ya Maneno

## Inadaiwa

Inasemekana, bila ushahidi, kuwa ulifanyika au kuwa na ubora maalum wa kinyume cha sheria au usiofaa.

## Shambulio

Shambulio la mwili linafafanuliwa katika Bodi ya Sera ya Elimu CR 4980 kama kitendo cha mwanafunzi kugusa kwa makusudi, kusukuma, kugonga au kujaribu kudhalimu mfanyakazi. Hii inatumika pia kwa tabia ileile kwa mwanafunzi mwingine.

Wilaya inajitolea kudumisha mazingira ya masomo na ya kufanya kazi yasiyo na aina yoyote ya shambulio la mwili. Kitendo chochote cha kimwili ambacho kinaumiza, au kina maana ya kumdhuru mtu mwingine katika mali ya shule au katika hafla ya shule, hakitaruhusiwa na kitashughulikiwa.

## Udhalimu

Udhalimu umefafanuliwa katika Sera ya 2655 ya Bodi ya Elimu kama hatua ya makusudi ya mtu au makundi ya watu ya kutoa vitisho, tabia ya fujo isiyohitajika, au ya unyanyasaji ambayo inajirudia au inaweza kurudiwa na inayomfanya mwanafunzi kuwa na hofu ya usalama wake wa kimwili au wa mali; ambayo hutatiza utendakazi wa elimu, fursa, au haki za mwanafunzi yeyote; au hutatiza shughuli za kawaida za shule. Udhalimu unaweza kujumuisha vitendo vya kimwili, vikiwemo ishara, au udhalimu wa maneno, kielektroniki, au mawasiliano ya kuandikwa, na tishio lolote la kulipiza kisasi kwa kuripoti vitendo vya udhalimu.

Wilaya imejitolea kudumisha mazingira ya kusoma na kufanya kazi yasiokuwa na aina yoyote ya udhalimu au vitisho kutoka kwa wanafunzi katika maeneo ya shule, wakati wa shule, katika shughuli zinazofadhiliwa na shule au katika muktadha unaohusiana na shule. Wanafunzi na/au wazazi/walezi wao wanahimizwa kuripoti matukio yoyote ya udhalimu kwa msimamizi wa jengo.

Wilaya inawahimiza wanafunzi kuripoti udhalimu. Wanafunzi wanapaswa kuripoti ikiwa hao ni waathiriwa au ni watazamaji. Shule zitajadili njia salama za kuripoti udhalimu na wanafunzi.

Wanafunzi wanaoonewa au kushuhudia maonevu wanapaswa kuripoti tukio hilo moja kwa moja kwa mtu mzima. Wazazi / walezi wanapaswa kuwasiliana na mwalimu mkuu ili kuripoti udhalimu ulioripotiwa na mtoto wao ikiwa mtoto hako sawa kutoa ripoti. Kila ripoti ya udhalimu itachunguzwa. Tovuti ya FHSD ina rasilimali za udhalimu kwa wazazi na wanafunzi chini ya Usalama na Ulinzi kwenye tovuti ya Wilaya.

## Mkutano

Mawasiliano ambayo hufanyika ana kwa ana, kwa video au kwa njia ya simu.

## Udhalimu wa mtandaoni

Udhalimu wa mtandaoni kama unavyofafanuliwa katika Sera ya 2655 ya udhalimu kama inavyofafanuliwa hapo juu kupitia upitishaji wa mawasiliano ikiwemo, lakini haijakomea kwa, ujumbe, matini, sauti au picha kwa njia za vifaa vya kielektroniki vikiwemo, lakini havijakomea kwa, simu, simu pasiwaya au kifaa kingine chochote cha mawasiliano pasiwaya, kompyuta, au peja. Huenda wilaya ikapiga marufuku au kuchukua hatua za kinidhamu kwa udhalimu wa mtandaoni ambao unatoka katika kampasi yoyote ya Wilaya au katika shughuli ya Wilaya ikiwa mawasiliano ya kielektroniki yalifanywa kwa kutumia rasilimali za kiteknolojia za shule, ikiwa kuna uhusiano wa kutosha na mazingira ya elimu, au ikiwa mawasiliano ya kielektroniki yalifanywa kwenye kampasi ya Wilaya au shughuli ya Wilaya kwa kutumia rasilimali za kiteknolojia za mwanafunzi binafsi. Isitoshe, wanafunzi wanaoshiriki katika vitendo vikubwa vya mienendo mibaya nje ya kampasi ambayo mwishowe huathiri pakubwa elimu ya wanafunzi wa Wilaya watachukuliwa hatua za kinidhamu.

## Uhalifu Mkubwa wa Wizi

Katika Missouri, wizi mbaya hufafanuliwa na kuainishwa chini ya RSMo Sehemu ya 570.030. Huenda ikawa uhalifu wa Class D au la C ikitegemea thamani ya mali au huduma zilizoibiwa. Uhalifu wa Class D hutokea wakati thamani ni $750 au zaidi, au ikiwa wizi unahusisha vitu maalum kama vile gari, wosia au silaha. Uhalifu wa Class C unashtakiwa wakati thamani ni $ 25,000 au zaidi.

## Unyanyasaji/Ubaguzi

Ni sera ya Wilaya kudumisha mazingira ya elimu ambayo hayana unyanyasaji kwa misingi ya mbari, rangi, jinsia, asili ya kitaifa, kabila, ulemavu, dini, mwelekeo wa kingono au mwelekeo wa kingono unaoshukiwa. Wilaya imepiga marufuku aina zote za unyanyasaji na ubaguzi kwa sababu za mbari, rangi, jinsia, asili ya kitaifa, jamii, ulemavu, dini, mapendeleo ya kingono au mwelekeo wa kingono unaoshukiwa.

Mfumo wa shule utachukua hatua mara moja ili kuchunguza malalamiko yote, yawe rasmi au yasiyo rasmi, ya kutamkwa au ya kuandikwa, ya unyanyasaji au ubaguzi kwa misingi ya mbari, rangi, jinsia, asili ya kitaifa, kabila, ulemavu, dini, mwelekeo wa kingono au mwelekeo wa kingono unaoshukiwa; mfumo huu utachukua hatua zinazofaa ili kuwalinda watu dhidi ya unyanyasaji au ubaguzi zaidi; na, ikiwa itabainishwa kwamba unyanyasaji au ubaguzi ulifanyika, kuchukua hatua za haraka na zinazofaa za kinidhamu dhidi ya mwanafunzi, mwalimu, msimamizi au mfanyakazi yeyote yule wa shule atakayepatikana kuwa alinyanyasa/kubagua, na/au kuchukua hatua nyingine mwafaka zinazofaa ili kukomesha unyanyasaji.

## Udhalilishaji

Udhalilishaji wa wanafunzi umepigwa marufuku kabisa na Sera ya Wilaya ya 2920. Udhalilishaji hufafanuliwa kama tabia ya kukusudiwa inayoelekezwa kwa mwanafunzi mwingine, iwe inatokea ndani au nje ya mazingira ya shule, kwa madhumuni ya kuanzisha au kuingia katika shughuli yoyote inayohusiana na shule au timu ya wanariadha. Maadili yaliyozuiwa na sera hii yanajumuisha, lakini hayajazuiwa kwa, ufichuzi au kugusa sehemu za siri, matako, au matiti (wanafunzi wa kike), moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kupitia kugusa nguo za ndani; vitisho vya madhara ya kimwili; na kuumiza au kudhalilisha kimwili au kiakili.

Wanafunzi watakaopatikana wamekiuka sera hii wataondoshwa kwa muda/kufukuzwa shuleni na kusimamishwa na kuzuiwa katika shughuli/ushiriki wa riadha kulingana na ukali wa tabia isiyokubalika.

## Hatari iliyo karibu

Hatari fulani, ya papo hapo, na inayokaribia; iliyo karibu sana, na inayotisha.

## Kuogopesha

Kuogopesha ni tabia ya kimakusudi ambayo ingemfanya mtu mwenye hisia za kawaida kuogopa kuumia au kuumizwa. Sio lazima kuthibitisha kwamba tabia hiyo ilikuwa ya ujeuri kiasi cha kusababisha hofu iliyosemwa au kwamba mwathirika alikuwa na hofu kweli.

## Uadilifu

Kitendo chochote cha kudanganya au kusema uwongo, iwe kwa maneno au bila maandishi, ikijumuisha kughushi.

## Vibali vya Kuegesha Gari

Kwa sababu ya nafasi isiyotosha ya wanafunzi kuegesha magari katika kila kampasi ya shule ya upili, vibali vya kuegesha magari vinahitajika kwa wanafunzi kuendesha magari shuleni. Kigezo cha kustahiki vibali na sheria nyingine zinazohusiana na magari ya wanafunzi zitawekwa na msimamizi anayefaa wa shule ya upili. Huenda ukiukaji ukasababisha kupoteza haki za kuegesha gari.

## Umiliki

Kuwa na kipengee kibinafsi au kwenye kabati la mtu, gari (ikiwa limeegeshwa kwenye eneo la wilaya), begi, mkoba au chombo kingine.

## Hali ya darasa iliyolindwa (unyanyasaji)

Hali yoyote inayofafanuliwa waziwazi na kulindwa na sheria ya shirikisho, jimbo au mtaa, kanuni au sheria, ikijumuisha jinsia, rangi, asili ya kitaifa, ukoo, imani, dini, ujauzito, hali ya ndoa, hali ya uzazi, mwelekeo wa kijinsia, utambuzi wa kijinsia, kujieleza kijinsia, au ulemavu wa kimwili, kiakili, kihisia, au kimasomo.

### Ununuzi

Kutoa pesa au ufikirio mwingine ili kubadilishana na dawa za kulevya, au ahadi ya kutoa pesa au jambo lingine baadaye ili kubadilishana na dawa.

### Urejeshaji

Kurudisha bidhaa ambazo ziliibwa au kuharibiwa au kutoa thamani nzuri ya soko kwa njia ya fidia au huduma.

### Jeraha kubwa la mwili

Jeraha kubwa la mwili ni madhara ya mwili ambayo husababisha moja au zaidi ya yafuatayo:
a. Hatari kubwa ya kifo;
b. Ulemavu au kasoro ya kudumu;
c. Kuzimia;
d. Hali ya kudumu au ya muda mrefu inayosababisha maumivu makali;
e. Hasara ya kudumu au ya muda mrefu au kuharibika kwa utendaji wa sehemu yoyote ya mwili; au
f. Matokeo yake ni kulazwa hospitalini.

Jeraha kubwa la mwili ni pamoja na, lakini sio tu, mifupa iliyovunjika au iliyokatika (ikijumuisha pua), na kupoteza fahamu. Jeraha kubwa la mwili halijumuishi macho meusi, makovu, mikwaruzo, au michimbuko.

### Tishio kubwa

Kujihusisha na mwenendo unaomweka mtu katika hofu ya madhara ya mwili, ikijumuisha, lakini sio tu, uchokozi/vitisho visivyo vya maneno, kauli za maneno au taarifa zilizoandikwa.

### Kutuma ujumbe wa kingono

Utumaji wa picha au ujumbe waziwazi wa kingono kupitia kifaa cha kielektroniki.

### Kugusana kingono

Kugusa yoyote, au kusababisha mtu mwingine kugusa, moja kwa moja au kwa njia ya nguo, sehemu yoyote ya mwili wa mtu yeyote, ikiwa inafanywa kwa nia ya kuamsha au kutosheleza tamaa ya ngono ya mtu yeyote, au kwa nia ya kunyanyasa, kudhalilisha, au kumshusha mtu yeyote.

### Kuiba/Wizi

Kuchukua au kujaribu kuchukua mali ya mtu au taasisi nyingine bila ruhusa au ufahamu wa mmiliki kwa lengo la kumnyima mmiliki matumizi yake (chini ya kosa la Wizi).

### Tishio kubwa

Tishio pale ambapo nia iko na hatua za ulinzi zinahitajika kuchukuliwa ili kumlinda mwathirika

(waathirika).

### Kudhihaki

Maneno ya kejeli, ishara, au matusi yanayokusudiwa kumkatisha tamaa mpokeaji, au kuwakasirisha na kuhimiza tabia za kujibu bila kufikiria.

### Silaha ya midoli

Midoli inayoiga silaha halisi, ikiwa ni pamoja na silaha za vita na bunduki zingine, lakini inakusudiwa kutumika kama bidhaa ya kuburudisha watoto na si hatari.

### Tishio la muda mfupi

Tishio ambalo ni kielelezo cha ucheshi, matamshi, hasira, au kufadhaika ambalo linaweza kutatuliwa kwa urahisi ili kusiwe na nia ya kudhuru. Hakuna tishio lililothibitishwa la madhara.

### Kupita bila ruhusa

Kuwa katika majengo ya shule bila ruhusa, ikiwemo wakati umeondoshwa kwa muda au kufukuzwa kabisa; pamoja na kuvunja na kuingia kwa nguvu. Au kubaki shuleni baada ya usimamizi wa shule kuomba mtu husika aondoke kwenye eneo la shule. Usimamizi wa shule utaomba maafisa wa kutekeleza sheria kumshtaki mwanafunzi, mzazi/mlezi, mshauri au mgeni kwa kosa la kupita bila ruhusa.

### Kutokuwa na ushirikiano/kutofuata sheria

Kukataa kushirikiana kunaweza kutokea wakati mwanafunzi anakataa kufuata sheria za shule au maagizo ya wafanyakazi wa shule au wajitoleaji kuna athari kwa utendaji mzuri au salama wa shule au darasa, kama vile kuendelea kubakia kwenye sehemu ya mapigano au kuchochea usumbufu baada ya kuambiwa aache tabia hiyo, au kutotii wafanyakazi wa shule mara kwa mara au wajitoleaji wakati mikakati mingine ya majibu haijafanikiwa kubadilisha tabia mbaya. Kutofuata sheria hakufanyiki wakati:

- Mwanafunzi hakuwa na ufahamu wa kutosha wa mwelekeo uliotolewa na wafanyakazi wa shule au anayejitolea (yaani, katika chumba chenye makelele, matatizo ya kusikia au ulemavu mwingine, vikwazo vya lugha, nk.);
- Mwanafunzi anachelewa kwenda shule/darasani;
- Mwanafunzi anakosa kukamilisha kazi ya ziada.

### Chini ya ushawishi wa kileo

Kuathiriwa na pombe au madawa ya kulevya kwa kiwango ambacho huzuia uwezo wa mtu kwa njia ambayo mtu wa kawaida angefanya.

### Vukivu

Inaweza kubadilika haraka na bila kutabirika, haswa kuwa mbaya zaidi.

### Silaha (ikiwemo vitu vinavyofanana na silaha na risasi)

Silaha ni, kwa njia ya maonyesho na bila kikomo, mojawapo ya zifuatazo:

- Bunduki: Bunduki kama inavyofafanuliwa katika sheria ya 18 U.S.C.921 ya serikali. Mifano ya bunduki inajumuisha bastola, bunduki ya marisau na bomu. Rejelea sheria ya serikali kwa ufafanuzi kamili.
- Bunduki Zingine: Bunduki ya aina yoyote, iwe ina risasi au haina risasi, inayofanya kazi au isiyofanya kazi, pamoja na kitu chochote kando na silaha ya vita ambacho kinafanana na bunduki. Hii itajumuisha, lakini haitakomea kwa, bunduki ya marisawa, bunduki ya rangi, bunduki ya kushtua, bunduki ya umeme, bunduki ya BB, bunduki ya fataki, bunduki ya misumari na bunduki ya hewa laini.
- Silaha Zingine: Chombo chochote au kitu kinachotumiwa kwa njia ya kutisha ambacho kinaweza kusababisha au kinakusudiwa kusababisha madhara ya mwili na/au jeraha, isipokuwa silaha ya vita au bunduki nyingine. Hii itajumuisha, lakini haijakomea kwa, kisu kinachoweza kubadilishwa, kisu cha kuwinda, kisu kama nyota, wembe (pamoja na wembe mnyoofu au wa kujirudisha ndani) vyuma vya ngumi, kikata sanduku, silaha yenye vijiti viwili, glavu zenye ncha, bambo la mkononi lenye ncha, rungu yoyote, kifaa cha kutoa machozi au bidhaa ya kunyunyizia maji yenye pilipili.

Sheria ya Jimbo la Missouri inayofafanua silaha inaweza kupatikana katika kiungo kifuatacho: Sheria ya Missouri